

pichani) juu ya umuhimu wa upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia juu kwenye ukurasa wa chini na mazuri

Mbegu bora madume ya ng'ombe yazaa matunda

Na Grace Mwakalinga, RUNGWE

UPATIKANAJI wa mbegu bora za madume ya ng'ombe kwa wafugaji wilayani Rungwe, mkoani Mbeya umechochea ongezeko kwa uzalishaji wa zao la maziwa kwa kuzalisha litu 200,000 kwa siku na kuingizwa sokoni.

Mwenyekiti wa Muungano wa Chama cha Wafugaji wilayani Rungwe (MUHAMARU), Asha Lukaja, alisema hayo kwenye elimu ya kutumia teknolojia za kisasa za ufu-

gaji kwa kuwatumia maofisa ugani waliosambazwa wilayani humo na Kampuni ya Asasi kwa kushirikiana na Serikali ya Denmack nchini Tanzania kwa lengo ya kuwavezesha wafugaji kuzalisha maziwa kwa tija na kuingiza katika mnyororo wa thamani.

Alisema kabila ya elimu hiyo waliitwa wakikabilwa na tatizo la masoko na mbegu bora, Kiwanda cha Maziwa cha Asasi kimewapattia madume ya mbegu bora za ng'ombe ambayo yamesaidia ongezeko la

majike na kuchoechea ongezeko la uzalishaji wa zao la maziwa.

"Licha ya ongezeko la uzalishaji wa maziwa na uwepo wa masoko ya uhakika bado tatizo kwa baadhi ya wafugaji kuingiza sokoni maziwa yaslyokuwa na ubora jambo lin-alochangia kuchafua na kutia doa maziwa yanayozalishwa wilayani Rungwe," alisema Lukaja.

Miongoni mwa wafugaji wilayani Rungwe, Fadhili Mbilinyi, alisema kuwapo kwa kampuni za ununuzi wa maziwa wilayani Rungwe kume-

leta tija wa wafugaji kuongeza uzalishaji na kufuga kisasa.

Alisema kwa sasa wanazalisha kiasi kikubwa cha maziwa na uhakika wa upatikanaji wa soko ndani na nje ya wilaya hiyo.

Ofisa Mifugo Wilaya ya Rungwe, Dk. Dennis Kamily, alisema wafugaji wengi hawapendi kuwatumia maofisa ugani kujifunza namna bora ya kuzalisha maziwa bila kutumia vyakula visivyo salama kwa ng'ombe.

Mkaguzi wa Maziwa Wilaya ya

Rungwe, Henry Mokiwa, alisema asilimia 20 ya maziwa yanayozalishwa na wafugaji wilayani humo yanakosa ubora kutoptana na baadhi ya wafugaji kuongeza maji.

"Ukamuaji wa maziwa kiholela kwa baadhi ya wafugaji kunachangia kuzalisha bakteria 500 hadi 1,000 kila baada ya saa tatu na kusababisha madhara kwa watumiaji na kushauri wafugaji kuwatumia maofisa ugani ili kuboresha sekta ya maziwa nchini," alisema Mokwa.

Mfumo mpya kukabili wizi wa mifugo

Bakari Kiang'o, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema mfumo wa kisasa wa kuvisha mifugo hereni katika usajili, utambuzi na kuweka alama utasaidia kupunguza changamoto za wizi wa mifugo.

Ndaki alieleza hayo jana wakati akizindua kiwanda cha kutengeneza hereni cha Kampuni ya S&J Animal Tech Ltd, kinachotengeneza mfumo huo unaotajwa kuwa wa kisasa zaidi katika kuweka alama za mifugo.

Awali, mifugo mbalimbali ikiwamo ng'ombe, mbuzi na kondoo ilikuwa ikiwekwa alama, utambuzi na kusajiliwa kwa njia kupiga chapa kwa kutumia chuma maalumu kinachowekwa katika moto, kisha kuwekwa kwenye ngozi zao.

Hata hivyo, njia hiyo illamikiwa na baadhi ya wafugaji waliodai mifugo yao hasa ng'ombe inaharibika hususan ngozi, lakini mfumo wa hereni wa kuvisha mifugo shingoni unatajwa kuwa bora zaidi.

Ndaki alisema suala matumizi ya mfumo wa hereni katika mifugo ni la msingi, huku akiwataka viongozi wa chama cha wafugaji walio-wakilisha wenzao katika uzinduzi huo kwenda kuwapa elimu hiyo.

"...mfumo huu pia utasaidia kudhibiti matukio ya wizi na mifugo. Naagiza ng'ombe wote wa Serikali kuwekwa mfumo huu," alisema Ndaki.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa wizara hiyo, Profesa Hezron Nonga alisema mfumo huo ni njia bora isiyoleta madhara kwa mifugo, akisema itahifadhi taarifa na hereni hizo zimetengenezwa kwa malighafi bora zaidi.